



**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII
CHUO CHA MISITU OLMOTONYI**

NAFASI ZA KUJIUNGA NA MASOMO YA MISITU KWA MWAKA WA MASOMO 2017/2018

Mkuu wa Chuo cha Misitu Olmotonyi anatangaza nafasi za masomo kwa mwaka wa masomo 2017/2018.

A. Mafunzo yanayotolewa

- i. Astashahada ya Misitu: (NTA - Level 5) Mafunzo ya miaka (2)
- ii. Stashahada ya Misitu: (NTA ó Level 6) Mafunzo ya miaka miwili (2)
- iii. Stashahada ya Misitu: (NTA ó Level 6) Mafunzo ya mwaka mmoja (1)

B. Sifa za Mwombaji:

I. Kozi ya Astashahada ya Misitu

- i. Mwombaji awe na cheti cha kuhitimu elimu ya sekondari.
- ii. Mwombaji awe amefaulu angalau masomo manne na ufaulu uwe kwa kiwango **cha D au zaidi**. Kati ya masomo hayo, lazima awe amefaulu mojawapo ya masomo ya Biolojia au Kemia au Fizikia au Sayansi ya kilimo au Jiografia. Ufaulu kwenye masomo ya Hisabati au Kingereza yatampatia mwombaji sifa ya ziada.

II. Kozi ya Stashahada kwa muda wa Miaka miwili

- i. Mwombaji awe na cheti cha kuhitimu elimu ya juu ya sekondari (kidato cha sita). Awe amefaulu angalau somo moja kwa kiwango cha E au zaidi katika mojawapo ya masomo ya; Biolojia au Kemia au Jiografia au Sayansi ya Kilimo na au Fizikia na subsidiari katika masomo mawili mengine

AU

Mwombaji awe na :

- (i) Astashahada ya Misitu (NTA level 5) aliyehitimu kwenye Chuo cha Misitu, Olmotonyi (FTI) kabla ya mwaka 2011.
- (ii) Astashahada (NTA Level 5) au stashahada (NTA Level 6) kutoka kwenye vyuo vinavyotambuliwa na Baraza linalosimamia Elimu ya Vyuo vya Ufundi (NACTE) vikiwa ni pamoja na; Chuo cha Mafunzo ya ufugaji wa Nyuki Tabora (BTI), Chuo cha viwanda vya mazao ya Misitu (FITI), Chuo cha Mafunzo ya Uangalizi wa Wanyama Pori (Mweka),; taasisi nyingine zinazotoa mafunzo ya sayansi ya Kilimo, Afya ya mifugo na Uzalishaji wa mazao kama vile, Chuo cha Mifugo na kilimo, Tengeru Arusha, Chuo cha Mifugo Mpwapwa (Wakala), Chuo cha Mifugo Morogoro, Chuo cha Mifugo Madaba, na Chuo cha Kilimo na Mifugo Kilacha (Moshi).

II. Kozi ya Stashahada kwa muda wa Mwaka mmoja

Mwombaji awe na :

- (i) Astashahada ya Misititu (NTA level 5) aliyehitimu kwenye Chuo cha Misitu, Olmotonyi (FTI) baada ya mwaka 2011.

C. ADA

Waombaji watakoachaguliwa watatakiwa kulipa ada kwa Mkuu wa Chuo kama ifuatavyo:

- i. Mwaka wa kwanza: Astashahada na Stashahada miaka miwili Sh 805,000/=
- ii. Mwaka wa pili: Sh 785,000/=
- iii. Stashahada mwaka mmoja: Sh 820,000/=

NB: Ada yaweza kulipwa kwa awamu mbili ó nusu ya ada mwanzo mwa kila Muhula .

D. MALAZI

Waombaji watakoapendelea kuishi kwenye hosteli za Chuo watapaswa kulipa Shs. 270,000/= kwa Mwaka lakini watalipia baada ya kujaza fomu za maombi ya hosteli na kujibiwa. Fomu zitaambatanishwa na barua ya kujiunga na Chuo.

- Angalizo:**
- i. Ada zinaweza kubadilika wakati wowote ndani ya kipindi cha mafunzo kadiri itakavyoonekana ni muhimu.
 - ii. Fedha ya kujikimu kwa chakula kiasi cha Tshs. 6,000/= au zaidi kwa kutwa moja

E. Jinsi ya Kutuma maombi

- i. Mwombaji atatakiwa kujaza fomu ya maombi ambayo italipiwa sh 30,000.00;
- ii. Maombi yote yaambatanishwe na vivuli vya vyeti halisi pamoja na nakala halisi slip ya benki.
- iii. Fomu za maombi zinapatikana Chuo cha Misitu Olmotonyi na kwenye Tovuti ya Chuo cha Misitu Olmotonyi, Arusha: [<http://www.fti.ac.tz>].

Ada na Malipo ya fomu yanapaswa kulipwa kupitia kwenye Akaunti ya Chuo; Jina la Akaunti ni : Mkuu wa Chuo Cha Misitu, Olmotonyi; Akaunti namba 40810041565, NMB Clock Tower.

F. Taarifa kwa watakoachaguliwa.

Majina ya watakoachaguliwa yatatangazwa kwenye magazeti ya kitaifa(Habari Leo na Daily news) na kwenye tovuti ya chuo (<http://www.fti.ac.tz>)

Kwa waombaji watakoahatika kuchaguliwa, watatumiwa maelezo ya kujiunga kupitia anuani na nambari za simu watakozokuwa wamezi bainisha kwenye anwani zao.

G. Tahadhari

Yeyote ambaye hatazingatia taratibu au mahitaji yaliyotajwa hapo juu maombi yake hayatafanyiwa kazi . Aidha, mwombaji atakayewasilisha taarifa za uongo akigundulika atachukuliwa hatua za Kisheria. Fomu zote za maombi zinatakiwa ziwe zimewasilishwa Chuoni kabla ya tarehe 20/08/2017. Maombi yatakawasilishwa baada ya tarehe hiyo hayatafanyiwa kazi.

Fomu za maombi zilizoambatanishwa na vivuli vya vyeti vya kuhitimu, vyeti vya taaluma na nakala halisi ya risiti ya benki (bank-slip) zitumwe kupitia anwani ifuatayo:

Mkuu wa Chuo,
Chuo Cha Misitu Olmotonyi,
S.L.P 943
Arusha.

Simu: Jumla :- +255-(027) 2509637
Moja kwa moja: +255-(027) 2505923
Nukushi : +255-(027)2509795

Barua pepe: info@fti.ac.tz
principal@fti.ac.tz
registrar@fti.ac.tz